UJUMUISHWAJI WA WANAWAKE KATIKA MCHAKATO WA BAJETI: MITANDAO YA WANAWAKE NA MAJUKWAA YA MAJADILIANO

MUHTASARI:
Taarifa hii fupi ya kisera inachambua ushirikishwaji na ujumuishwaji wa majukwaa ya wanawake, mitandao na ushirika mwingine ya wanawake katika mchakato wa bajeti Tanzania. Makala inawasilisha uchambuzi wa kina, na mambo yaliyoibuliwa, yanayohusu umahiri wa mitandao hiyo katika mchakato wa bajeti.

MAMBO MAKUU YALIYOIBULIWA:

- Kuna uelewa mdogo, ushirikishwaji na ujumuishwaji hafifu wa majukwaa ya wanawake, mitandao, ushirika na makundi mbalimbali ya wanawake katika mchakato wa bajeti. Wanawake wa vijijini wanashiriki na wana uelewa zaidi wa mchakato wa bajeti kuliko wanawake wa mijini.
- Majukwaa/mitandao yenye mahusianao ya karibu au iliyoanzishwa na Serikali ni imara zaidi, ukilinganisha na ile isiyokuwa na mahusiano ya karibu na Serikali au majukwaa ya majadiliano ya ngazi ya juu kitaifa.
- Kuna uwajibikaji mdogo katika mchakato wa bajeti kuhusu kupanga, kuidhinisha, kutekeleza na ufuatiliaji.
- Ajenda ya wanawake haijitokezi wazi na wala mijadala na ajenda ya kitaifa haijumuishi vya kutosha masuala ya wanawake; sauti zao hazisikiki.
- Hakuna mfumo wa wazi wa majadiliano na uwakilishi wa pamoja wa wanawake; jambo linalopunguza ushirikiano, muunganiko na uwezo wa kujenga ajenda ya pamoja, mashirikiano na ubia mkakati.
- Majukwaa ya majadiliano na mitandao, kama taasisi, haina taratibu na mifumo mizuri ya usimamizi na wala uwezo wa kirasilimali fedha na watu.
- Majukwaa ya wanawake/mitandao na wawakilishi wao hawana uwezo wa kufanya uchambuzi wa kina na kujumuisha masuala ya wanawake katika shughuli nyingine za kiuchumi na hivyo kuwapunguzia uwezo wa kujenga hoja zenye mashiko.

MAPENDEKEZO YA KISERA:

- Kufanya kampeni za kinamama ili kuhamasisha na kuongeza uelewa wa pamoja na kujenga uwezo wa kujumuisha jinsia katika mchakato wa bajeti katika ngazi zote.
- Kuhamasisha watumishi wa serikali kuu na serikali za mitaa ili waandae bajeti zinazozingatia usawa wa jinsia na kuzawadia watendaji wazuri.
- Kukuza uwezo wa kitaasisi, wa majukwaa ya wanawake, mitandao na ushirika wao na kujifunza kutokana na uzoefu wa mradi wa “BEST-Dialogue.”
- Taasisi za juu za kitaifa kama vile TPSF na TNBC kwa kushirikiana na Serikali wanapaswa kutoa msaada na kusaidia kujenga uwezo wa vikundi vya wanawake ili kuboresha uratibu na kujenga ushirika mkakati baina yao.
- Kuna haja ya kujifunza kutokana na uzoefu wa majukwaa mbalimbali na mitandao tofauti, na vilevile kujenga ushirikiano mzuri na taasisi nyingine katika nchi zinazoendelea, kupitia mitandao na majukwaa ya majadiliano ya kimataifa.
- Serikali inapaswa kuanzisha kituo kikuu cha mawasiliano, kitakachochochea usawa, uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji wa wanawake na vijana, katika mchakato wa bajeti.
- Kuna haja ya kuboresha utaratibu wa usajili, na sheria, ili kurahisisha urasimishaji wa majukwaa, mitandao na vikundi vya wanawake.

Co-funded by the European Union

1. UTANGULIZI NA USULI

Kuwa na mipango shirikishi, na mchakato wa bajeti unaojumuisha makundi yaliyotengwa na jamii, wakiwemo watu wenye ulemavu, vijana na wanawake, ni jambo linalojadiliwa na jamii na katika nchi nyingi. Inachukuliwa kwa ujumla kwamba watu wengi wanaelewa mchakakto wa bajeti na kwa hiyo watashiriki katika utelezaji wake. Lakini kwa kawaida bajeti inakuwa wazi tu baada ya kuidhinishwa na Bunge. Kuna ushiriki mdogo wa wadau wakati wa maandalizi yake na hata katika utekelezaji, ufuatiliaji na thathmini.
Taarifa hii fupi ya kisera inaelezea mambo yaliyoibuliwa katika utafiti ulioichambua kwa kina bajeti ya serikali, yaani “Tanzania’s Fiscal Governance, Budget, Needs and Public Expenditure With the Analysis on Inequalities and Trust." Katika utafiti huu wanawake viongozi, na baadhi ya wajumbe wa majukwaa mbalimbali ya majadiliano, mitandao na vikundi vya wanawake walihojiwa. Makala haya yanatoa kwa muhtasari mambo makuu yaliyojitokeza na mapendekezo ya vikundi vilivyohojiwa kuhusu uelewa wa ushiriki wao, na namna wanavyojumishwa katika mchakato wa bajeti Tanzania. Taarifa inawasilisha sauti za wanawake kuhusu mchakato wa bajeti kwa kulinganisha mambo yaliyojitokeza katika majukwaa na mitandao yao mbalimbali.

2. MAJUKWAA NA MITANDAO YA WANAWAKE NA USHIRIKA MWINGINE TANZANIA

Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2012 za “National Bureau of Statistics (NBS)”, wanawake ni asilimia 49.7 ya watu wote Tanzania. Kwa hiyo ni muhimu kujumuisha sauti zao katika bajeti. Majukwaa ya wanawake ya majadiliano, mitandao na vikundi vyao ni vingi na vya aina tofauti vikiwa na wajumbe tofauti. Vikundi vingine vimeandikishwa rasmi na vingine sio rasmi. Majukwaa mengi ya majadiliano, mitandao na vikundi hivi vimeanzishwa kwa maslahi ya wajumbe wake, na vinalenga kusukuma mbele ajenda zao. Wengi wanafanya kazi tu katika ngazi ya taifa lakini wana wajumbe wachache kutoka mikoani, wilayani na katika ngazi za chini zaidi.
Mapitio ya majukwaa, mitandao na vikundi, inaonesha tofauti ya wazi kati ya vikundi hivi.
Kwanza, ni vikundi ambavyo vina mahusiano ya karibu na majukwaa ya juu ya kitaifa kama vile TNBC na TPSF au majukwaa ya kisekta kama ACT, CTI na TCCIA nk., na Serikali Kuu au wizara za kisekta. Vikundi hivi vingi vimeandikishwa rasmi lakini ni idadi yake ni ndogo.
Kundi la pili, ni vikundi ambavyo havina uhusiano na majukwaa ya juu, vingi vikiwa ni vikundi vya wanataaluma. Katika Makala haya tunalinganisha utendaji wa majukwaa na mitandao ya wanawake ambayo ina mahusiano ya karibu na majukwaa ya juu kitaifa na Serikali (mfano TWCC, TAP, TAWLAE, TGNP) na ile ya wanataaluma ambayo haina mahusiano na majukwaa ya juu na Serikali (mfano TAMWA, TAWECE, TAWCA) na mwanamke mmoja mmoja.

2.1 Mitandao ya Wanawake Wanataaluma na Washirika Wasio na Mahusiano na Majukwaa ya Juu Kitaifa na Serikali

Hii ni mitandao ya wanawake na vikundi ambavyo vingine vimeandikishwa rasmi lakini vikundi vingi havikujiandikisha rasmi. Na wote hawana mahusiano ya moja kwa moja na majukwaa ya juu kitaifa, wala wizara za Serikali, Idara au Mawakala wa serikali (MDAs).

MITANDAO NA VIKUNDI VYA WANAWAKE WANATAALUMA WASIO NA MAHUSIANO NA MAJUKWAA YA JUU NA SERIKALI
Wanawake wanataaluma wa Tanzania: Hii ni mitandao/vikundi vinavyowakilisha wanawake wanataaluma kama wahasibu (TAWCA) na wanasheria (Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA). TAWCA ni jukwaa la wanawake wahasibu wabobezi na wahasibu wengine. Wajumbe ni watumishi wa serikali, kutoka katika sekta binafsi na wanafunzi; na wengi wako Dar es Salaam na Dodoma. Pia kuna wajumbe wanaowakilisha mikoa kama mabalozi. Mtandao huu ulianzishwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu (NBAA), na wanapata msaada kutoka NBAA na Wizara ya Fedha. TAWLA inawakilisha wanawake wanasheria, ilianzishwa na wajumbe wenyewe.
Ushirika wa Wanahabari Wanawake: Tanzania Media Women Association (TAMWA) ni mtandao wa wajumbe waliojiandikisha kama asasi isiyokuwa ya kiserikali (NGO). Wajumbe wanatoka serikalini, sekta binafsi, na wanahabari mmoja mmoja. Uwakilishi wao uko katika ngazi ya kitaifa tu, Dar es Salaam na Dodoma. Mtandao huu una mahusiano ya karibu na Wizara ya Mawasiliano na Utamaduni na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wanawake, Wazee na Watoto. Wajumbe wanashiriki mikutano mingi ya serikali na majukwaa mengine kama wanahabari. Mtandao huu umewahi kualikwa kujadili bajeti.

PILOT4 RESEARCH AND DIALOGUE · Tampere University · Pilot4DEV · IMED · COWI · Co-funded by the European Union

2.2 Majukwaa na Mitandao ya Wanawake Wenye Mahusiano na Majukwaa ya Juu Kitaifa na Serikali

Haya ni majukwaa yenye mahusiano na mitandao ya juu kitaifa. Wengi wao wameandikishwa rasmi na uwakilishi unapitia TPSF, TNBC, ACT, TCCIA. Vikundi hivi ni pamoja na:

MITANDAO NA VIKUNDI VYA WANAWAKE WENYE MAHUSIANO NA MAJUKWAA YA JUU KITAIFA NA SERIKALI
Majukwaa, Mitandao na Vikundi wa Wanawake Wajasiriamali: Wakiwakilishwa na - Tanzania Women Chamber of Commerce (TWCC); Tanzania Food Processors Association (TAFOPA); Federation of Association of Women Entrepreneurs (FAWETA); Tanzania Women Miners Association (TAWOMA); the African Women's Entrepreneurship Program (AWEP); Tanzania Women Entrepreneurs Network, na Development Exposition (TWENDE); na the Coalition for Advancement of Women in Agriculture Tanzania (CAWAT), Tanzania Growth Trust (TGT), Nronga Women Diary Cooperative (WOMEN IN DIARY), Muungano wa Vikundi vya Usindikaji (WODSTA), VICOBA Feta nk. Ni TWCC pekee, ndiyo ina uwakilishi katika ngazi ya mikoa; na katika ngazi ya taifa uwalikilishaji wake unapitia Tanzania Private Sector Foundation (TPSF).
Ushirika wa Wanawake Viongozi: Tanzania Association of Women Leaders in Agriculture and Environment (TAWLAE) ni ushirika ulioandikishwa kama Asasi isiokuwa ya kiserikali (NGO). Ushirika huu ulianzishwa na serikali ukiwa na wajumbe kutoka serikalini, sekta binafsi na mtu mmoja mmoja. Uwakishi wake upo katika ngazi ya taifa na mikoa wakiwatumia sana maafisa ugani wa kilimo. Ushirika huu unajuisha Tanzania Agriculture Council (ACT), Agriculture Non-State Actors Forum (ANSAF), Policy Forum (PF), Tanzania Chamber of Commerce Industry Agriculture (TCCIA) na TPSF.
Wanawake Katika Sekta ndogo ya Ufugaji wa Kuku: Tanzania Poultry Association (TAP) ni jukwaa la majadiliano la wanawake wafuga kuku na wanaotoa huduma katika sekta hii. Uwakilishi wake unapitia maafisa watendaji wakuu (CEOs) round table (CORT), TPSF, TCCIA, Poultry Breeders Association (PBA), Agriculture Annual Policy Conference (AAPC), Tanzania National Business Council (TNBC), Kinondoni Business Council na Africa Women Agribusiness (AWA).
Wanawake Mainjinia: Tanzania Women Engineers Convention and Exhibition (TAWECE) ni ushirika wa majadiliano wa wanawake mainjinia. Ushirika huu unafanya kazi katika ngazi ya taifa tu kupitia taasisi ya Mainjinia (apex organization) na unapata msaada kutoka Wizara ya Kazi na TPSF. Ushirika huu haujawahi kualikwa katika mchakato wa bajeti, kama wanawake mainjinia. Kama mainjinia wanaona jukumu lao la msingi ni shughuli za ujenzi wa miundo mbinu na kazi nyingine za kiinjinia na hawaoni jinsi wanavyoweza kuchangia masuala ya wanawake; wakati kuna masuala kama namna barabara na umeme vijijini vinavyoweza kusaidia shughuli za wanawake katika maeneo ya vijijini.
Mtandao wa Jinsia wa Wanawake: Tanzania Gender Networking Platform (TGNP) siyo taasisi ya muundo wa wajumbe, bali ni mtandao unaohamasisha ujumuishwaji wa masuala ya wanawake katika shughuli za taasisi mbalimbali na kuziwajibisha. Mtandao huu unafanya kazi katika ngazi ya taifa ukiwa na wahamasihaji kupitia halmashauri za mitaa. Mtandao hauna uwakilishi katika mitandao ya juu kitaifa (apex representation). Mtandao umekuwa ukushughulikia masuala ya maji, elimu, fedha na afya kupitia wizara husika. Na siku za karibuni wameanza kushughulikia kilimo.

3. MUHTASARI WA MAMBO YALIYOIBULIWA

Kwa ujumla kuna uelewa mdogo, na ushirikishwaji hafifu wa majukwaa ya wanawake ya majadiliano, mitandao, ushirika na vikundi mbalimbali vya wanawake katika mchakato wa bajeti. Vilevile hakuna uwajibikaji kwa wanawake, na ni shida kupata nyaraka za serikali. Wanawake waishio vijijini wana mwamko mkubwa zaidi na wanashiriki katika mchakato wa bajeti zaidi, ukilinganisha na wanawake wa mijini. Sehemu zifuatazo zinalinganisha makundi mawili ya wanawake katika ushiriki, ushirikishwaji, uwajibikaji, uwazi, imani na kufikiwa.

PILOT4 RESEARCH AND DIALOGUE
Tampere University
Pilot4DEV
IMED
COWI
Co-funded by the European Union

3.1 Ushirikishwaji, Ujumuishwaji na Uwajibikaji

Utafiti unaonesha kwamba kuna uelewa na ushirikishwaji mdogo katika mchakato wa bajeti. Vilevile hakuna mifumo na taratibu za wazi za uwajibikaji.

Mitandao na Vikundi vya Wanawake Wataaluma Wasio na Uhusiano wa Karibu na Majukwaa ya Juu ya Majadiliani Kitaifa na Serikali (mfano, TAMWA, TAWECE, TAWCA)	Majukwaa ya Wanawake/Mitandao Yenye Uhusiano wa Karibu na Majukwaa ya Juu ya Majadiliano Kitaifa na Serikali (mfano, TWCC, TAP, TAWLAE, TGNP)
Ushirikishwaji: Kuna uelewa mdogo wa mchakato wa bajeti na ushirikishwaji mdogo – hawajawahi kualikwa kushiriki	**Ushirikishwaji:** Masuala ya wanawake hayajadiliwi na hayajumuishwi katika bajeti zinazoidhinishwa. Vilvile hakuna utaratibu wa wazi wa majadiliano, uwakilishi, usajili na kuna sheria kandamizi.
Ujumuishwaji: masuala ya wanawake hayajadiliwi na hayajumuishwi katika bajeti zinazoidhinishwa. Vilvile hakuna utaratibu wa wazi wa majadiliano, uwakilishi, usajili na kuna sheria kandamizi.	**Ujumuishwaji:** masuala ya wanawake hayajadiliwi na hayajumuishwi katika bajeti zinazoidhinishwa. Vilvile hakuna utaratibu wa wazi wa majadiliano, uwakilishi, usajili na kuna sheria kandamizi.

Uwajibikaji: Hakuna dhamira na nia thabiti ya wabunge, ya kusukuma mbele ajenda ya maendeleo ya wananchi. Aidha kuna uelewa mdogo wa majukumu ya viongozi wa Serikali kuanzia ngazi za chini hadi taifa, katika mizunguko ya kibajeti. Kwa maana hii ni vigumu kuwajibika. Vilvile kuna mazoea ya jamii -wakiwemo wanawake, kuchukulia bajeti kama jambo la kisiasa na hivyo wanakosa ari ya kushiriki. Kwa ujumla, kuna utata katika mchakato wa uwajibikaji. Serikali na majukwaa ya juu kitaifa kama TNBC, TPSF, CTI na wengine, bado hawajaweka juhudi ya kutosha kusukuma mbele ujumuishwaji wa masuala ya wanawake katika mchakato wa bajeti, na kukuza uelewa kwa majukwaa ya wanawake, mitandao, ushirika na vikundi vya wanawake. Maafisa bajeti wa Wizara, Idara kuu na Wakala wa Serikali na hata wabunge, hawana ujuzi na uwezo wa kutosha kupanga, kuandaa bajeti na kufanya uchambuzi unaozingatia usawa wa jinsia. TGNP na TWCC wameanza kukuza uelewa kuanzia ngazi za chini vijijini. Pamoja na kwamba mchakato wa bajeti ni wa muda mrefu wanawake wanalalamika kwamba muda wake na hasa jinsi jamii inavyoweza kushiriki havieleweki kwa wanawake wengi; na zinahitajika jitihada za makusudi serikalini, kuhakikisha ushiriki wao. Kwa ujumla, wanawake wengi wanachukulia mchakato wa bajeti kama shughuli ya maafisa wa serikali tu.

"BAJETI NI KAZI YA SERIKALI NA SIO YA WANANCHI WA KAWAIDA, PIA HAKUNA USHIRIKISHWAJI WA MOJA KWA MOJA NA HUWA HAITILIWI MKAZO KAMA INAVYOKUWA KWENYE UCHAGUZI WA VIONGOZI WA SIASA".

Viongozi na watumishi wengi wanaoendesha shughuli za kila siku za mitandao na ushirika wa wanawake wanafanya kazi kwa kujitolea – jambo linalopunguza ufanisi. Mitandao mingi ilianzishwa kupitia wafadhili/miradi ya wafadhili, utaratibu ambao ni vigumu kuuendeleza baada ya miradi kukamilika.

3.2 Uwazi, Imani na Kufikiwa

Kuna malalamiko kuhusu uwazi katika mchakato wa bajeti na utaratibu mzima wa mawasiliano.

Mitandao na Vikundi vya Wanawake Wataaluma Wasio na Uhusiano wa Karibu na Majukwaa ya Juu ya Majadiliani Kitaifa na Serikali (mfano, TAMWA, TAWECE, TAWCA)	Majukwaa ya Wanawake/Mitandao Yenye Uhusiano wa Karibu na Majukwaa ya Juu ya Majadiliano Kitaifa na Serikali. (mfano, TWCC, TAP, TAWLAE, TGNP)
Uwazi: Baadhi ya nyaraka za serikali ni za siri. Masuala ya wanawake hayajumuishwi katika bajeti. Kuna haja ya kulenga masuala mahsusi ya wanawake.	**Uwazi:** Baadhi ya nyaraka za serikali ni za siri.

Imani: Katika makundi yote mawili hakuna bajeti inayojulikana wazi kama bajeti ya kutekeleza/kufuatilia utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa kwa masuala ya wanawake; mfano, taulo za wanawake. Pia, wawakilishi hawana ujuzi wa kiuchambuzi na kiutafiti; ikiwa ni pamoja na uwezo wa kujumuisha masuala ya wanawake katika shughuli za kiuchumi, mipango na bajeti. Aidha, wanakosa timu ya ushindi (champions) ya kusukuma mbele ajenda ya wanawake.

PILOT4 RESEARCH AND DIALOGUE · Tampere University · Pilot4DEV · IMED · COWI · Co-funded by the European Union

Kufikiwa: Kwa pande zote mbili baadhi ya nyaraka za bajeti hazipatikani kirahisi na zinazopatikana ni kubwa mno na zinapatikana tu katika tovuti ya serikali na hivyo wanawake wengi hawawezi kuzipata. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba wajumbe na mitandao, majukwaa, ushirika na vikundi vya wanawake na pia wanawake mmoja mmoja, hawawaamini wawakilishi wao kwani hawatoi mrejesho kwa wajumbe wenzao na hivyo kuchangia sauti za wanawake kutosikika. Malalamiko makubwa ni:-

- Masuala ya wanawake hayajadiliwi au kupewa kipaumbele wakati wa mchakato wa bajeti. Hakuna bajeti inayotengwa kwa ajili ya masuala ya wanawake au hata kufuatilia utekelezaji wa masuala ya wanawake. Mfano mzuri ni suala la taulo za wanawake kukosa suluhisho endelevu.
- Sauti hazisikiki hata pale wanaposhirikishwa katika mijadala ya majukwaa makuu na mitandao ya kitaifa. Uwakilishi wao ni zaidi wa kuonekana kushiriki badala ya masuala ya wanawake kupewa umuhimu stahiki.
- Majukwaa ya wanawake/ mitandao/ushirika vinakosa timu ya ushindi ya kusukuma mbele ajenda zao.

4. MAJUMUISHO

Uchambuzi linganishi wa majukwaa ya majadiliano ya wanawake, mitandao, vikundi na mwanamke mmoja mmoja unaonesha kwamba mchakato wa bajeti siyo shirikishi, jumuishwaji na wazi. Jitihada za ushirikishwaji zinakwazwa na uelewa na uwezo mdogo wa washiriki. Majukwa mengi ya Juu ya majadiliano hayana uwezo na uelewa wa kuchambua bajeti na taratibu zake za utekelezaji. Vilvile wanakosa rasilimaili watu na fedha za kuwawezesha kushiriki kikamilifu wakati wanapoalikwa. Hii inadidimiza jitihada za programu za uhamasishaji na hivyo kupelekea sauti za wanawake kutokusikika. Masuala ya wanawake hayawasilishwi vizuri katika bajeti.

5. MAPENDEKEZO KUTOKA KATIKA MAJUKWAA NA MITANDAO YA WANAWAKE, WASHIRIKA NA MTU MMOJA MMOJA

Ili kuongeza ushirikishwaji na ujumuishwaji wa masuala ya wanawake katika mchakato wa bajeti majukwaa ya majadiliano ya wanawake/ mitandao yao/vikundi na mwanamke mmoja mmoja wanapendekeza yafuatayo:

- Kuwepo na kampeni kwa jamii ya kukuza uelewa na ushirikishwaji wa hiari katika mchakato wa bajeti na mipango elekezi ya muda mrefu.
- Kuboresha upashanaji habari. Kwa sasa kuna taarifa finyu mno kuhusu mchakato wa bajeti na namna na kushiriki katika mchakato huo.
- Kujenga kujiamini na uwezo wa kuchambua na kufanya tathmini ya mipango na bajeti.
- Kuimarisha taratibu za kutoa mrejesho kutoka katika majukwaa/ mitandao na viongozi wa taasisi, kwa wajumbe wao, kabla na baada ya mchakato wa bajeti na kuhakikisha masuala ya wanawake yanapewa umuhimu stahiki katika mipango ya kitaifa na bajeti.
- Majukwaa yote, mitandao na taasisi zinapaswa kuwa na programu za kujenga uwezo wa kupanga na maandalizi ya bajeti ili kuwawezesha kujumuisha masuala ya wanawake katika mipango na bajeti.
- Kuna haja ya majukwaa ya majadiliano ya wanawake, mitandao na vikundi mbalimbali kuunda umoja utakowaunganisha wanawake wote na kuwawezesha kuwa na ajenda ya pamoja ya wanawake.

MTAFITI MKUU
Prof. Marcellina Mvula Chijoriga ni profesa mstaafu wa mambo ya fedha na menejimenti ya biashara. Alihudumu katika Taasisi ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (University of Dar es Salaam Business School -UDBS) kwa miaka 36. Ni mkufunzi mbobezi, mtafiti na mshauri mtaalamu wa biashara za umma na binafsi. Pia alikuwa mjumbe wa bodi mbalimbali na taasisi kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania na Shirika la Fedha Duniani -IMF. Kwa sasa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa kampuni ya LOGIMAC Ltd.

PILOT4 RESEARCH AND DIALOGUE
Tampere University
Pilot4DEV
IMED
COWI
Co-funded by the European Union